

FORM 4 TERM 1 END TERM EXAMS-2020

FASIHI YA KISWAHILI

MUDA: SAA 2¹/₂

MAAGIZO:

1.Jibu maswali MANNE Pekee.

2.Swali la kwanza ni la lazima.

3.Maswali mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki.

4.Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

5.Kila swali lina alama ishirini

FORM 4 TERM 1 END TERM EXAMS-2020

FASIHI YA KISWAHILI

1.SHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)

Eti

Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi

Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa

Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki

Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe

Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi

Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu

Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii

FORM 4 TERM 1 END TERM EXAMS-2020

FASIHI YA KISWAHILI

Wala si makaratasi, siondoki

Maswali

- a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)
- b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)
- c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
- d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)
- e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)
- f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
- g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
- h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 3)
- (i) Karatasi
- (ii) Nimesaki
- (iii) kitovu

2 SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

- a. Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)
- b. Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (al. 4)
- c. Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. (al. 2)
- d. Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjeelea tamthilia. (al. 10)

3. wa kurejelea tamthilia ya 'Kigogo ya Pauline Kea, onyesha jinsi ambavyo viongozi wengi katika nchi za kiasia wamejawa na tamaa. (alama 20)

SEHEMU C. RIWAYA YA CHOZI LA HERI (ASSUMPTA MATEI)

4. "Kwa kweli ni hali ngumu hii"

Weka dondoo katika muktadha wake.

(alama 4)

Ni hali gani yamsemewa inayorejelewa kwenye dondoo.

(alama 16)

5) Ukabila ni tatizo sugu katika nchi nyingi za Kiafrika. Tetea kauli hii ukilejelea Choji la Heri

(al. 20)

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine
jibu swali la 6 au la 7**

FORM 4 TERM 1 END TERM EXAMS-2020

FASIHI YA KISWAHILI

6. Ukirejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza.
(alama 20)

- a) Mapenzi ya kifaurongo
- b) Masharti ya kisasa
- c) Ndoto ya Mashaka
- d) Mtihani wa maisha

Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad

7. "Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine?"

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa za msemaji. (alama 6)
- c) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

- 8a) Fafanua mchakato/fomula ya uwasilishaji wa vitendawili. (alama 4)
- b) Linganisha naulinganue vitendawili na methali. (alama 10)
- c) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. (alama 6)